

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO
TAASISI YA SANAA NA UTAMADUNI BAGAMOYO
(TaSUBa)**



**MAOMBI YA KUJIUNGA NA CHUO KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018
KWA MUHULA UTAKAOANZA APRILI 2018**

Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (Zamani Chuo cha Sanaa Bagamoyo) anakaribisha maombi ya kujiunga na Chuo kwa kozi za Astashahada (Cheti) na Stashahada (Diploma) katika fani zifuatazo.

- i. Sanaa za Maonyesho na Ufundi (Performing and Visual Arts) - Muziki, Ngoma, Uigizaji, Sarakasi, Ufundi wa Jukwaa (Stage Technology) na Sanaa za Ufundi (Fine Art).
- ii. Picha Jongevu (Film and TV Production) - Uchukuaji wa Video (Video Shooting), Kuhariri Video (Video Editing), Kuongoza Filamu (Film Directing) na Uandishi Miswada ya Filamu (Script Writing).
- iii. Uzalishaji wa Muziki na Sauti (Music and Sound Production) - Kurekodi Sauti (Sound Recording), Kurekodi Muziki (Music Recording), Uzalishaji wa Muziki (Music Production) na Usimamizi wa Studio (Studio Management).

1. CHETI MWAKA MMOJA (One year Certificate – NTA 4)

SIFA ZA KUJIUNGA

Mwombaji anatakiwa awe na sifa ifuatayo;

- Aliyemaliza kidato cha Nne (**FORM IV**) na kupata Ufaulu wa kuanzia “D” Nne (4).

2. STASHAHADA (Two year Diploma – NTA 6)

SIFA ZA KUJIUNGA

Mwombaji anatakiwa awe na sifa moja wapo kati ya hizi zifuatazo;

- Awe amehitimu kidato cha Sita (**FORM VI**) na kupata Ufaulu wa kuanzia Principal Pass Moja (1) na Subsidiary Moja (1).
- Awe amehitimu ngazi ya Astashahada (Cheti NTA 4) kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na NACTE.
- Awe amehitimu kozi ya Ualimu **Grade A**.

MAELEZO MENGINE

- Maombi yote yatumwe moja kwa moja Chuoni kwa kujaza FOMU ya maombi ambayo inapatikana Chuoni na kwenye tovuti ya Taasisi www.tasuba.ac.tz.
- Gharama ya maombi ni **Tsh.10,000/=** na malipo haya yatafanyika kupitia **BANK** ya **NMB** Akaunti Na. **21001100012** na jina **UTAWALA CHUO CHA SANAA**. Stakabadhi ya malipo (Receipt/Bank Pay Slip) itaambatanishwa pamoja na maombi ya kujiunga na Chuo.
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **30/03/2018**.
- Kwa mawasiliano zaidi tumia anwani zifuatazo; **MTENDAJI MKUU, TaSUBa, S.L.P 32, BAGAMOYO**, AU Barua pepe taasisisanaa@gmail.com AU tasuba@habari.go.tz AU kwa kupitia namba za simu; +255 (0)23 2440032, 0763408792, 0655840405, 0713297626, 0715974100 au 0683993401.